



ULINZI KWA MTOTO KILA MTOTO ANA HAKI YA KULINDWA

9 Shiriki mashindano ya uandishi wa insha, uchoraji mabango yenye ujembe kuhusu watoto

3 TFFT ikitoa mafunzo kwa walimu wa Jiji la Arusha katika mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunza

14 Jifunze hatua mbalimbali za makuzi na malezi ya mtoto

Tafiti nyingi zinaonesha kuwa Tanzania ni moja ya nchi zenye kiwango cha juu cha unyanyasaji wa watoto katika ngazi za familia, shuleni na jamii kwa ujumla. Tumeshuhudia jinsi watoto wanavyo kosa haki zao za misingi kama haki ya ulinzi na usalama.

Sisi kama shirika tuna amini kwamba mtoto anapaswa kulindwa dhidi ya vituvyote hatarishi, uonevu, kunyonywa, kudhalilishwa, kufedheheshwa, kuteswa, kudhulumiwa, kubaguliwa au kutekwa na kutoroshwa. Ili kuhakikisha ulinzi na usalama kwa mtoto, tumetoa mafunzo ya ulinzi kwa mtoto kwa maafisa wa ustawi wa jamii wa wilaya ya Meru na halimashauri ya jiji la Arusha.



Ni wazi kwamba washiriki hawa wanauwezo na mchango mkubwa katika kuhakikisha mtoto wa kitanzania analindwa dhidi ya hatari mbalimbali kwani kundi hili mara nyingi hufanya kazi au kujihusisha na watoto moja kwa moja. Katika kutimiza lengo hili washiriki wameweza kujua kiwango cha unyanyasaji dhidi ya watoto nchini Tanzania, na kuchunguza mitizamo yao wenyewe kuhusu nini maana ya unyanyasaji. Pia kujua majukumu yao katika kulinda watoto chini ya sheria za Tanzania na kimataifa.



Licha ya kwamba swala la ulinzi wa mtoto kuwa ni la jamii nzima. Wao kama wataalumu na watu ambaye hukaa na kufanya kazi na watoto kwa muda mwingi kuliko makundi mengine katika jamii inatakiwa wawe mstari wa mbele katika kuhakikisha ulinzi

wa watoto. Mfano, katika mazingira ya shule mwalimu anawajibu mkubwa wa kuhakikisha mtoto ambaye ni mwanafunzi yupo katika hali ya ulinzi na usalama lakini kwa wakati mwingine tumeona wazi watoto wengi wakifanyiwa vitendo vya kikatili wakiwa mashuleni.

Kama tukitafakari kwa kina kuhusu madhara ya ukatili na unyanyasaji tulio fanyiwa sisi wenyewe katika maisha yetu au hata mtu mwingine tunaweza tambua kuwa swala hili ni la msingi sana. Pia nilazima jamii yote ijue kwamba ni rahisi sana kumjenga mtoto kuliko kumrekebisha mtu mzima kwani mtoto wa leo ndio mtu mzima wa kesho. Hivyo ilikuwa na jamii imara inatulazimu kulinda rasilimali yetu muhimu sana ambaye ni watoto wetu.



Mbali na athari za ukatili dhidi ya watoto kwa ajili ya maendeleo mapana ya nchi, washiriki waliweza kuchunguza asili ya tabia binafsi wanazokuwa nazo waathirika wa unyanyaswaji. Wameweza kutambua jinsi gani sheria zinawalinda watoto wa Tanzania, taratibu na kanuni

ambazo hutoa mwongozo wa namna ya kuripoti na kukabiliana na kesi ya ukiukwaji wa haki za watoto.

Kadhalika katika jamii kuna mitazamo mbalimbali tunapo zungumzia swala la ulinzi na haki za mtoto. Ni vyema kutumia fursa hii kueleweshwa uma na jamii kwa ujumla kwamba haki za ulinzi na haki za mtoto zipo kwa dhana kuu kwamba chochote kinachofanyika katika hili ni kwaajili ya maslahi bora ya mtoto. Na si vinginevyo kama vile kumpa mtoto kujiamulia na kufanya kama anavyo taka, sisi kama wazazi au walezi wa watoto wetu bado tunafasi yetu katika kuhakikisha makuzi na malezi mema ya watoto kwa kuhakikisha ulinzi bora na kuzingatia haki zao za msingi.

TFFT kama shirika tunaamini kwamba watoto wote wanahaki sawa katika jamii, wanapokuwa shuleni au nyumbani na ili kufanikisha adhma hii tunajenga uwezo wa watoa huduma kwa watoto kupitia mafunzo mbalimbali ikiwemo hili la ulinzi kwa mtoto.

Pia kama shirika tunashiriki kwa namna mbalimbali katika kumlinda mtoto. Hii ni pamoja na kuanzisha masanduku ya Furaha na Huzuni (Happy and Sad Boxes) kwa shule za wilaya ya Meru. Kwa kupitia masanduku haya wanafunzi huweza kueleza kwa kuandika mambo ambayo ni mazuri na huwafurahisha pia mambo ambayo sio mazuri na kuwa

huzunisha katika maisha yao ya kila siku wakiwa shuleni au nyumbani na chombo husika kuchukua hatua stahiki.

Mwisho ninapenda kutoa wito kwa watu binafsi, serikali, mashirika binafsi na wadau wote wa watoto kuungana nasi katika kuhakikisha ulinzi wa mtoto na haki zao za msingi zinazingatiwa wakati wote.

**Chapisho na : Noah Kayanda
Teacher Training Program
Coordinator**

Mafunzo kwa Walimu wa Jiji la Arusha 2016



Shirika la The Foundation for Tomorrow limewezesha mafunzo kwa walimu wa halimashauri ya jiji la Arusha tarehe 17 mwezi wa 5 mwaka huu wa 2016. Mafunzo hayo kwa walimu yamefanyika katika kituo kikuu cha walimu

cha wilaya, Kijenge Teachers Resource Center (TRC) kilichopo katika shule ya Kijenge msingi. Tofauti na walimu walio shiriki mafunzo pia wadhhibiti ubora kutoka jiji la Arusha walipata kushiriki mafunzo haya. Wawezeshaji katika warsha hiyo walikuwa ni waratibu wa kituo cha walimu Kijenge ambaye walisha pata mafunzo kupitia warsha zilizo andaliwa na kuwezesha na TFFT mwanzoni mwa mwaka huu.

Mafunzo hayo kwa walimu yalijikita katika mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunza kwa walimu na wanafunzi. Tafiti mbalimbali za kielimu zinaonyesha kwamba mwanafunzi wanapaswa kufikia malengo, kupata ujuzi na maarifa mapana kujenga kumbumbu ya kudumu, ubunifu na kuamsha hisia na ari ya kujifunza ndani na nje ya darasa endapo mwanafunzi atajifunza au kufundishwa kwa njia shirikishi.



Kama ajenda kuu ya mafunzo haya walimu wameweza kupata ujuzi na maarifa katika mbinu mbalimbali ambazo ni shirikishi. Wameweza kujifunza ni kwanamna gani na wakati gani wanaweza kuzitumia njia hizi za kufundishia katika mazingira mbalimbali.

Warsha hii ambayo ilikuwa na washiriki mafunzo, walimu kutoka shule mbalimbali katika halimashauri ya jiji la Arusha ilitupatia fursa ya kujifunza kutoka kwa wengine na kupata uzoefu na maarifa mapya katika swala la kufundishia na kujifunza hususa ni kwa kutumia mbinu shirikishi. Kwa ujumla ilikuwa ni mafunzo ya kipekee yenye hamasa kwa kila mmoja wetu kuwa na shahuku kujifunza jambo jipya katika swala zima la ufundishaji.

Kupitia warsha hii ya mafunzo kwa walimu tunategemea kupata mabadiliko makubwa katika nyanja ya elimu. Sisi kama walimu tulioshiriki mafunzo na hatimaye kuandaa mpango mara baada ya mafunzo haya, tunatazamia kufundisha wanafunzi kwa kutumia mbinu shirikishi ndani na nje ya darasa, kutambua na kuwa na nafasi kubwa katika ufundishaji na kujifunza. Kukidhi shauku na matarajio makubwa ya kutoa na kupokea maarifa, stadi, ujuzi na mwelekeo baina ya mwalimu na mwanafunzi.

Hivyo kupitia mafunzo haya tunatarajia mabadiliko makubwa kwa walimu walio shiriki mafunzo kwa kuwafundisha vyema wanafunzi katika shule zao husika.



Kuhakikisha ubora wa elimu ni moja ya mambo muhimu zaidi tunaweza kufanya kwa ajili ya watoto wetu na maendeleo kwa taifa letu la Tanzania.

Lakini ikumbukwe kwamba hakuna elimu bora pasipo na walimu bora siku zote mbali na

rasilimali zingine za kufundishia na kujifunzia walimu wana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha wanafunzi wanapata maarifa, ujuzi na uzoefu ambao ni bora na wenye kukidhi mahitaji ya jamii katika viwango vya juu

Tunalishukuru shirika la TFFT, kwa kulitambua hilo nakuchukua hatua madhubuti za kuwekeza kwa walimu kwa kutoa mafunzo mbali mbali ili kuboresha kiwango cha elimu katika shule zetu.

Mwl, Eliud V. Chang'a
Mratibu wa Kituo cha Walimu Jiji
la Arusha.



Life Skills Corner

By: Hilda Lema
Full Circle Program Manager

Mikutano ya Robo mwaka na waalimu wa Somo la Haiba na Michezo walioko katika mradi. Januari, April and Julai 2016

Mikutano ilipangwa kufanyika mara tatu kwa mwaka kujadili maendeleo ya mradi wa Haiba na Michezo. Katika mikutano hii, waalimu waliohudhuria mafunzo ya Haiba na Michezo waliudhuria mara zote; Tulijadili mafanikio ya mradi, vizuizi, mikakati, matumizi ya dhana za kufundishia na dhana za michezo.

Matumizi ya mtaala na shughuli katika kufundisha Haiba na Michezo, Mabadiliko yaliyopelekewa na mradi wa somo la Haiba na Michezo.

Shule 12 zipo katika mradi huu wa majaribio ambao unaelekea ukingoni. Shule hizo ni: Maua, Upendo Academy, Tanzania Adventist, Sylus Anderson, Sinai, Leguruki, Maji ya Chai, Kimandafu, Leganga na Chemchem. Kipindi cha mwanzo kulikua na changamoto kubwa kama, waalimu kutotumia mtaala saidizi na vifaa vya michezo kwa sababu hawakujua umuhimu wake.

Baada ya vikao vya mara kwa mara na maelekezo ya kutosha jinsi ya kutumia shughuli za mafunzo zilizopo kwenye mtaala waalimu waliona umuhimu wa kuutumia. Waalimu wameona mtaala huu mpya unamrahisishia mwalimu katika ufundishaji, umeboreshwa na kurahisishwa, umeelekeza kila mada inavyopaswa kufundishwa na kila mada ina shughuli za mafunzo za kufundishia ukilinganisha na mtaala wa serikali. Sanduku la vifaa tulilotoa pia lina vifaa vya kutosha kufundishia somo la haiba na michezo.

Tuna wajengea uwezo watoto kwa kuwafundisha stadi na ujuzi muhimu ili kuweza kustawi katika maisha yao



Waalimu wakiwa kwenye kikao cha robo mwaka, Aprili 2016

Mafanikio katika Mradi wa Haiba na Michezo

Umeboresha mahusiano kati ya waalimu na wanafunzi (wanafunzi wanakua huru kuuliza maswali yanayowakabili katika changamoto za ujana na mpito kwa waalimu).

Wanafunzi wamepata fursa ya kujua mambo mengi ambayo wazazi au shuleni hawakua na muda wa kujadili au kuzungumzia.

Mtaala una shughuli nyingi za mavunzo za kufundishia kila mada na maelezo ya kutosha jinsi ya kufundishia.

Wanafunzi wanapenda somo la haiba na michezo kwa kuwa katika hili somo wanajifunza stadi za maisha na uhalisia wake. Somo hili linafanya wanakua wabunifu, wajasiriamali na wenye kutaka kujua mambo. Pia linawasaidia kujua jinsi ya kukabiliana na changamoto za maisha.

Mtaala mpya wa haiba na michezo unampa mwalimu ujasiri na kujiamini katika kufundisha Somo la Haiba na Michezo

Somo limeibua vipaji vingi vya wanafunzi kutokana na vifaa vya michezo walivyopatiwa. Wanafunzi wengi hawajabarikiwa kitaaluma lakini kupitia vifaa vya michezo tumeweza kugundua wana vipaji vingine.

Changamoto

- Baadhi ya mada vifaa havikuwepo vya kufundishia na kujifunzia, mfano kete.
- Sanduku la vifaa halikuwa na kisanduku cha huduma ya kwanza, wanafunzi wakiumia wanakosa huduma hapo kwa hapo.
- Japo darasa la saba wanapaswa kufundishwa Haiba na Michezo baadhi ya shule zimefuta hili somo kwa kisingizio kuwa darasa la saba wanakua katika maandalizi ya mwisho.
- Baadhi ya shule za serikali zina watoto elfu moja, vifaa vilivyotolewa havikidhi mahitaji.

Mafunzo ya kuanzisha klabu za stadi za kazi mashuleni

Baadhi ya shule waliomba mafunzo ili waweze anzisha klabu zitakazosaidia wanafunzi katika maswala mazima ya stadi za maisha. Mafunzo yalitolewa kwa shule saba wilaya ya Meru na Arusha Morden. Waalimu walikubalia baadhi ya shughuli ambazo wanafunzi wanaweza kufanya ambazo hazitagharimu fedha. Shule zilizoshiriki mafunzo ni Sinai, Sylus Anderson, Maua, Upendo, Usa River, Arusha Modern na Tanzania Adventist.

Klabu hizi zitasaidia watoto kujijengea tabia za ujasiri, tabia za ujasiriamali, kujitegemea, kuweza

kuwasiliana kwa ufasaa, kukabiliana na maisha bila kusubiri au kutegemea kuajiriwa, kujitambua na kuwa viongozi wa mfano. Kila shule iliyoshiriki waliangalia shughuli inayowezekana kufanyika shuleni kwao kulingana na mazingira. Baadhi ya klabu zitakua zinajishughulisha na haya yafuatayo: uchoraji, mpira, bustani na upandaji miti na mboga mboga, ususi, kupika maandazi, karanga, Midahalo na kadhalika.

Mafunzo ya Matumizi ya Muda na Kuandaa ratiba ya kujisomea Arusha Modern

Wanafunzi wa Shule ya Arusha Modern walipata fursa ya mafunzo ya siku tatu yaliyotolewa na Full Circle Program kutoka TFFT. Mafunzo haya yalikuwa na malengo ya kuongeza kiwango cha ufaulu na kutunza muda kwa wanafunzi. Wanafunzi walijifunza utunzaji wa muda na kuandaa ratiba za kujisomea. Tuliwaongoza ni jinsi gani muda ni wa thamani, namna ya kutumia kila dakika wakiwa shuleni au nyumbani. Pia tuliwasaidia kila mmoja kuandaa ratiba yake ya kujisomea kulingana na kila somo.



Ili akili ifanye kazi vizuri wanahitaji mapumziko, baada ya mapumziko na kujihusisha katika shughuli wanazoagiziwa kufanya basi wanaweza kutulia na kujisomea. Tumegundua kuwa wanafunzi

wengi waashindwa kujiwekea utaratibu mzuri wa kujisomea. Mwongozo walioupata umewasaidia kujua mbinu za kujisomea na muda mwafaka. Pia wanafunzi walipata fursa yakutushirikisha kazi wanazopenda kufanya baadae. Tulichukua muda huo kuwashauri masomo yanayoendana na kazi wanazotaka kufanya ili waongeze bidii na kuongeza shauku ya kuchunguza kutoka kwa watu walioko katika fani hizo.



Swala la michezo halikusahaulika, walishiriki katika michezo mbali mbali iliyohitaji ubunifu wao, walipenda sana hiyo michezo ikiwemo kutengeneza na kupanga maumbo ya wanyama mbali mbali kama chui, twiga, simba na tembo. Kuvuka mto wenye mamba bila kukanyaga maji, mbio za kijiko na michezo mingine. Tungependa shule zote ziwe na nafasi ya kushiriki katika shughuli kama hizi. Zinafungua sana uelewa wa wanafunzi na kila mwanafunzi anapata mda wa kushiriki vyema.



Tunatoa wito kwa waalimu kuwa wabunifu katika kufundisha,

watumie mbinu shirikishi ili kuweza kutambua uelewa wa kila mtoto darasani. Hii itawasaidia kuelewa nguvu wanayopaswa kuongeza ili kuwasaidia wale ambao hawafanyi vizuri.

Mradi wa Full Circle Program unalenga wanafunzi ambao wamefunzwa na kujifunza stadi za maisha vyema shuleni. Ujuzi unaopatikana utawasaidia kukabiliana na maisha pindi wanapokua wamemaliza masomo. Wanapata fursa ya kujifunza namna ya kuwasiliana kwa ufasaha, mbinu za ujasiriamali, mahusiano, maadili na utu, haki za watoto, Mimba na njia za uzazi salama, Kubalehe na kadhalika. Hii ni misingi ambayo watoto wanapaswa kujua ili waweze kuishi vyema na kukabiliana na changamoto za ujanani.

Mashindano ya Uandishi bora wa Insha: Julai 2016 Wilaya ya Meru, Arusha.

TFFT kupitia mradi wa Full Circle Program tunalenga kuandaa wanafunzi ambao wanauwezo wa kujitegemea na kuwa huru na kushirikiana na jamii zao kutatua matatizo yanayokabili jamii zao. Tunaamini katika elimu inayogusa nyanja zote za maisha ya mwanafunzi ambayo inazidi yale

anayofundishwa darasani.

Mwaka huu tunadhamini mashindano baina ya shule za msingi wilaya ya Meru na Arusha mjini yanayotarajia kushirikisha wanafunzi kuanzia darasa la 4-7. Kutakua na mashindano 3: Kuandika insha (Kiingereza na Kiswahili), Kutengeneza mabango yenye ujumbe tofauti unaohusiana na watoto, Zawadi ya fedha taslimu na vyeti zitatolewa kwa washindi watatu wa mwanzo kwa kila shindano watakaochaguliwa na jopo la waamuzi.

Mambo ya Kuzingatia:

1. Mashindano haya yatafanyika tarehe 13-15 Julai. Sherehe za kukabidhiwa zawadi zitafanyika tarehe 22, Julai 2016.

2. Mashindano haya yanakaribishwa kwa shule zote za msingi za serikali na binafsi kutoka Arusha manispaa na Wilaya ya Meru.

3. Kila shule itayoshiriki inapaswa kuwa na mshiriki mmoja kwa kila shindano.

4. Kila shule itakayoshiriki lazima walipe kiingilio cha shilingi elfu 10,000, itakayotumika kugharamia matumizi ya mashindano haya.



Psychosocial and Health Corner

By: Hedwiga Mchaki
Psychosocial and Health
Program Manager

Makuzi na Malezi kwa Mtoto.

Katika kutambua umuhimu wa malezi kwa watoto shirika liliandaa semina ya siku tatu kuhusu malezi ya mtoto. Semina hii ililenga kuwaelimisha waratibu wa elimu kata, maafisa ustawi wa jamii kutoka halimashauri ya jiji la Arusha na wilaya ya Meru. Pia shule washirika wa TFFT na wafanyakazi wa shirika la TFFT tuliweza kushiriki katika mafunzo haya.



Nia hasa ni kupata uelewa wa hatua mbalimbali za makuzi na malezi ya mtoto ili kuweza kuwahudumia watoto tukiwa tunajua ni hatua gani wapo katika makuzi yao na wanahitaji msaada gani waweze kupita vyema katika hatua hizo. Waliohudhuria semina hii walipewa majukumu ya

kufikisha ujumbe huu kwa jamii pana zaidi ili kuweza kukuza uelewa wa jamii yetu katika malezi na makuzi ya watoto.

Ni wazi kwamba washiriki wa semina hii wanasehemu kubwa sana katika jamii kwenye kuhakikisha elimu hii ya makuzi na malezi kwa mtoto inafikia jamii kwa mapana zaidi kama ilivyo kusudiwa.

Washiriki wameweza kujifunza mambo mengi na ya msingi kwa habari ya makuzi na malezi ya mtoto. Kwa mfano, Makuzi ya mtoto mwenye umri wa siku moja mpaka miezi 36. Tumeweza kuangalia ukuaji wa mtoto, kimwili, kiakili, kimahusiano na watu wengine na ukuaji wa kihisia. Kwa kawaida maeneo haya manne yanategemeana ili kumwezesha mtoto kukua kwa ujumla.

Kwa mfano ili mtoto akue kimwili, anahitaji ukuaji wa akili ipasavyo ambayo nayo itaathiri namna anavyomudu hisia zake na hivyo kuhusiana na watu wengine. Kwa hiyo ni sawa tukisema hakuna ukuaji wa eneo moja usiotegemea eneo jingine.

Ukuaji wa kimwili

Kwa kawaida ukuaji wa mwili kwa mwaka wa kwanza huenda kwa kasi kubwa. Kwa mfano, wakati mtoto huzaliwa akiwa na wastani wa uzito wa kilo 3.4 hivi, ndani ya

miezi sita uzito huo huongezeka mara dufu na kufikia mara tatu anapotimiza miezi 12. Hii ni kasi kubwa inayotegemea sana ubora wa lishe, mazingira rafiki ya ukuaji, afya ya mwili na hata nasaba za ukuaji alizorithi mtoto kutoka kwa wazazi wake wawili. Ili kuwezesha ukuaji huu kufanyika, mtoto hulala usingizi mfupi mfupi kwa masaa kati ya 16 na 18 kwa siku. Kulala hutokea mchana kuliko usiku lakini kadri anavyokuwa usingizi huanza kutokea wakati wa usiku kama ilivyo kawaida ya wengi.



Kwa muda wote wa miaka mitatu ya mwanzo, kwa ujumla, mtoto huwa bado akijifunza kuvimudu viungo vya mwili wake na kuvitumia kwa usahihi ili aweze kukabiliana na changamoto za kimazingira. Kinywa ndiyo sehemu inayomsisimua mtoto kipindi hiki. Kila anachoshika, safari yake huishia kinywani. Usafi na uangalizi wa karibu unahitajika vinginevyo anaweza kujikuta akipata magonjwa yatokanayo na uchafu.

Ni katika kipindi hiki ndipo mtoto huweza kuimudu shingo yake vizuri, mikono na kiwiliwili na hivyo anapotimiza miezi sita huwa tayari ana uwezo wa kuhama mwelekeo akiwa usingizini. Asipoangaliwa vizuri mzazi anapostuka usingizini usiku wa manane anaweza kumwokota mtoto akiwa uvunguni.

Baada ya kumaliza miezi sita, mtoto huanza kuota meno kwa

mkupuo wa meno mawili mawili yakianza kwenye ufizi wa chini na kisha ufizi wa juu. Ni wakati huo huo ambapo mtoto huanza kukaa mwenyewe hatua kwa hatua kisha ndani ya miezi 12 ya mwanzo huanza kutambaa, kusimama na hatimaye kuchukua hatua ya kwanza kabla au baada tu ya mwaka wa kwanza.

Kuwekeza katika makuzi na maendeleo ya watoto wetu kuanzia umri wa mwanzo ni moja kati ya jambo muhimu na la pekee ambaye jamii tunaweza fanya.

We want to hear from you! If your school has newsworthy events, projects you are proud of, or thoughts you want to share that you would benefit your fellow educators and other school managers, send them to us and we will publish them in the next edition of Tufundishane! Articles that talk about best practices will be given preference, but we also welcome literary contributions such as, essays and poems from educators and students.

For comments or suggestions, email:
noah@thefoundationfortomorrow.org

or message/ call: +255 753 661 770

Physical address:
2nd floor king Solomon house Anglican Church compound



This year the foundation for tomorrow (TFFT) is celebrating its tenth year. For a decade TFFT'S work can be encapsulate in one word- "THRIVE." Our work is about empowering Most Vulnerable Children (MVC) to thrive and reach their fullest potential and contribute to improving their communities.

Through our Scholarship Program, Psychosocial and Health Program, Teacher Training Program and Full Cycle Program, most vulnerable children thrive into the actualization of this reality in their lives.

We would love for the local community in Tanzania to participate in this pursuit. Together we can address the challenges the children face and ensure their access to quality education and the medical care, safeguard their wellbeing ensuring they are free from harm and abuse and equip them with all the necessary skills they need to thrive. There are so many ways you can help.

SCHOLARSHIP PROGRAM

Provide most vulnerable children access to quality education.

PSYCHOSOCIAL AND HEALTH PROGRAM

Provide access to healthcare and improve MVC household Economic Strengthening Project (Wezeshu Kaya).

TEACHER TRAINING PROGRAM

Equip teachers with necessary skills to deliver quality instruction.

FULL CIRCLE PROGRAM

Equip children with necessary life skills for them to thrive in life.

YOU CAN BE A PART OF TFFT STORY.

We welcome donations in cash or kind to help us expand the reach of our programs. And if you feel you can make a positive impact on youth's life coaching or mentoring, we would love to hear from you!

Web: www.thefoundationfortomorrow.org
Email: info@thefoundationfortomorrow.org
Face book: [TheFoundationForTomorrow](https://www.facebook.com/TheFoundationForTomorrow)
Twitter: [@TFFTAFRICA](https://twitter.com/TFFTAFRICA)